



TAARIFA KWA UMMA

UTARATIBU WA ULIPIAJI WA HUDUMA ZINAZODHIBITIWA

Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), katika kutekeleza majukumu yake ya udhibiti wa huduma katika sekta ya usafiri majini, linawaelekeza watoa huduma wanaodhibitiwa kuwa malipo kwa ajili ya huduma zinazotolewa kwa wateja mbalimbali yanaweza kufanyika kupitia Dola ya Kimarekani (United States Dollar) au kiwango kinacholingana katika Shilingi za Kitanzania (Tanzania Shillings).

Ileweke kuwa sarafu ya kitanzania ni fedha halali na mtu au taasisi yoyote haipaswi kukataa kupokea malipo katika fedha hiyo. Aidha, Serikali ilikwisha kutoa maelekezo kuhusu matumizi ya Sarafu ya Kitanzania katika kufanya malipo ya bidhaa na huduma zitolewazo katika soko la ndani.

Kwa msingi huu, wateja wapatao huduma katika sekta ya usafiri majini nchini wana uhuru wa kufanya malipo ya huduma kwa shilingi za Kitanzania au Dola ya Kimarekani.

Watoa huduma wanaelekezwa kuzingatia maelekezo haya.

Mkurugenzi Mkuu

TASAC

06 Juni, 2023